**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(KITUO JUMUISHI CHA HAKI KATIKA MASUALA YA MIRATHI NA NDOA)**

**ILIYOPO TEMEKE**

**RUFAA YA MADAI NA. 34 YA 2023**

(Inatokana na hukumu ya Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Kituo Jumuishi, inayoketi Temeke, Katika shauri la Rufaa ya Ndoa Na. 98 ya 2022)

**FATMA SAID JUMA............................................................ MRUFANI**

**DHIDI YA**

**LUKOLO JUMA BIMBA...................................................... MRUFANIWA**

# HUKUMU

19 Aprili & 22 Mei 2024

**JAJI BARTHY.:**

Hii ni rufaa ya pili iliyoletwa na Fatma Said Juma ambae ni Mrufani dhidi ya Lukolo Juma Bimba ambaye ni Mrufaniwa. Wadaawa hawa waliwahi kufunga ndoa ya Kiislamu mnamo tarehe 16/9/2017 na kubarikiwa kupata mtoto mmoja.

Asili ya rufaa hii inatokana na shauri la Talaka Na. 292 la 2022 kutoka katika Mahakama ya Mwazo Temeke, Kituo Jumuishi cha Mirathi na Ndoa ambapo mrufani alikuwa mdai, aliyepeleka maombi dhidi ya mdaiwa ambaye sasa ni mrufaniwa akiomba talaka, mgawanyo wa mali na matunzo ya mtoto. Sababu ya kuomba ndoa yao ivunjwe ilikuwa ni mrufani kupewa talaka ya kidini na mrufaniwa.

Mahakama iliridhika kuwa ndoa ya wadaawa imevunjika kiwango cha kutokuweza kurekebishika, iliamriwa talaka itolewe ikiambatana na amri ya mgao wa mali. Iliamriwa mrufani alipwe Tsh. 3,500,000/= kama fidia ya

pango la nyumba aliyopanga baada ya kutelekezwa na matunzo ya mtoto yatolewe baada ya gari aina ya Vits yenye nambari ya usajili T.788 DSY kuuzwa na Mrufaniwa apewe 40% ya mauzo na 60% kwa mrufani. Gari hiyo ikiwa ni mali pekee ya wanandoa hao.

Mrufaniwa hakuridhishwa na maamuzi hayo ndipo alikata rufaa Kwenda katika Mahakama ya Wilaya iliyoko pia Kituo Jumuishi (mahakama ya kwanza ya rufaa). Ambapo baada ya kusikiliza rufaa hiyo, Mahakama iliamuru mrufani alipwe fidia jumla ya kiasi cha shilingi Tsh. 5,250,000/= ikiwa ni pango na fidia ya matunzo ya jumla ya Tsh. 3,250,000/= kwa muda wa miezi 21.

Mrufani kadharika hakuridhishwa na maamuzi ya rufaa ya kwanza, alipinga maamuzi hayo kwa kukata rufaa katika Mahakama hii kwa sababu zifuatazo;

1. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutozingatia utofauti wa namba ya shauri la ndoa kwenye hukumu na wito wa tarehe 03/03/2022.*
2. *Kwamba, mheshimiwa hakimu alisiyekiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutotoa uamuzi wa kukataa nyaraka za mauziano zilizobadilishwa tarehe za manunuzi na taarifa ya viwanja hivyo.*
3. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutoa amri ya kulipwa kwa stamp duty badala ya kutozingatia mikataba ya mauziano iliyotolewa kama kielelezo ikiwa haijalipiwa stamp duty.*
4. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutozingatia maelezo*

*yaliyotolewa na mashahidi upande wa mdai wa mdaiwa ambayo yalibadilishwa kwenye hukumu ya shauri la ndoa.*

5. *Kwamba, mheshimiwa hakimu alisiyekiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutokuamuru mgao wa machumo ya ndoa kwenye uwiano sawa kutokana na ukweli kwamba mrufani na mrufaniwa walikuwa waaajiriwa.*
6. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutotambua kwamba mrufani amechangia katika maboresho ya mali za mrufaniwa.*
7. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutotoa amri ya kufanyika vipimo vya DNA kulingana na mamlaka yake.*
8. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutozingatia vielelzo vilivyotolewa na mrufani kuthibitisha upatikanaji wa mali za ndoa na maboresho yake.*
9. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kutoamuru usikilizwaji upya wa shauri kuwapa mafasi mashahidi walioitwa na mahakama ili kuthibitisha upatikanaji wa mali za ndoa na maboresho yake.*
10. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kuamuru fidia ya kodi ya nyumba iliyopaswa kuwa shilingi 8,670,000/= sawa na miezi 36 kuanzia kutelekezwa hadi tarehe ya hukumu ya madai ya talaka.*
11. *Kwamba, mheshimiwa hakimu aliyesikiliza shauri la rufaa ya ndoa amekosea kimantiki na kisheria kwa kuamuru fidia ya*

*matunzo ya mke iliyopaswa kuwa shilingi 5,400,000/= sawa na miezi 36 kuanzia kutelekezwa hadi tarehe ya hukumu ya talaka.*

Hivyo, mrufani anaiomba mahakama itupilie mbali hukumu ya mahakama ya wilaya na kuamuru usikilizwaji upya wa shauri la ndoa mbele ya hakimu mwingine, kuamuru mashahidi walioshindwa kusikilizwa wasikilizwe na kupokea nyaraka za ushahidi uliokataliwa na nafuu nyingine ambazo mahakama inaona zinapaswa kutolewa.

Shauri hili lilisikilizwa kwa njia ya maandishi, pande zote zilileta hoja zao kwa wakati, isipokuwa mrufani hakuleta hoja zake za majumuisho.

Katika mawasilisho makuu ya mrufani yaliandikwa na wakili Emmanuel Richard Machibya. Alianza na sababu ya 10 na alieleza kwamba, mahakama iliyosikiliza rufaa ilikosea kwa kuamuru mrufaniwa alipwe fidia ya fedha ya kodi ya nyumba Tsh. 3,500,000/= kwa miezi 21 kutoka Juni 2019 hadi tarehe ya hukumu ya Shauri la Nndoa Na. 271 ya mwaka 2021 badala ya miezi 36 kiasi cha Tsh. 5,250,000/=. Mrufani pia alipinga uamuzi ulioeleza mkono fidia ya kodi isitokane na mauzo ya gari Vitz iliyosajiriwa kwa namba T.788 DSY.

Pia alisistiza kuwa mahakama ya wilaya ilikosea kwenye kuhesabu ambapo ilitoa amri fidia ianze mwezi Machi, 2021 ilipotolewa talaka ya tatu kwa mujibu wa dini ya Kiislamu.

Akiendelea na mawasilisho, Bw. Machibya alijumuisha sababu ya 5, 6 na 8 pamoja na kueleza kwamba, mahakama ya kwanza ya rufaa ilikosea kimantiki na kisheria kwa kutoamuru mgawanyo sawa wa machumo, kutozingatia maboresho aliyochangia mrufani na kutozingatia vielelezo vinavyothibitisha upatikanaji wa mali za ndoa na maboresho.

Alirejea kifungu cha 9(3) cha Sheria za Ndoa, Sura ya 29, Iliyorejewa 2019, ambacho kinatambua ndoa ya mke zaidi ya mmoja kama mojawapo ya aina moja wapo ya ndoa.

Pia kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) (b) na kifungu 10(2)(a) cha Sheria ya Ndoa, katika ndoa ya kiislamu ya wake wengi izingatie mchango wa kila mke katika upatikanaji wa ndoa. Alieleza ndoa ilifungwa tarehe 16/09/2017 ingawa Mahakama ya Mwanzo ilidai ndoa ilifungwa 2007.

Wakili Machibya alisema pia ni makosa kwa kutogawa mali zote kwa usawa kama kifungu 60(a)(b) cha Sheria ya Ndoa kielekezavyo ingawa ukweli ni kwamba kuna mali zilipatikana kabla ya ndoa na nyingine zilipatikana wakati wa ndoa. Ilikuwa ni rai yake kuwa mali zilizopatikana kabla ya ndoa zilikuwa na malengo ya kutumika katika ndoa, hivyo mahakama isibague mali za mrufaniwa iwe imepatikana katika ndoa ya mke mmoja au ndoa ya wake wengi, mali hizo zigawiwe kwa usawa.

Aliendelea kueleza kwamba mrufaniwa alishirikiana na mrufani katika ujenzi wa ghorofa moja iliyojengwa katika nyumba anayoishi na mke wa kwanza na alitoa mchango wa Tsh. 750,000/= ushahidi ambao haukutiliwa mkazo na mahakama. Alieleza zaidi kuwa kuna magari matatu na mashamba ambayo mrufani alinunua akiwa na mrufaniwa, lakini vielelezo vilikatakiwa na mahakama na ilikataa kutoa nyongeza ya muda mrufani alete mashahidi wake.

Wakili Machibya akijadili sababu ya 3 alidai mikataba ya mauziano ambayo ilikuwa kama kielelezo haikulipiwa udhuru wa forodha "stamp duty". Hakimu wa Mahakama ya Wilaya katika ukurasa wa 2 wa hukumu alikubaliana na hoja ya wakili kwamba mikataba iliyotolewa ilikinzana na kifungu 47(1) cha Sheria ya Ushuru wa Forodha (Stamp Duty Act), Sura ya 189, iliyorejewa 2019. Pia ilijielekeza vibaya kuangalia maamuzi ya kesi ya **First National Bank(T) Ltd dhidi ya Yohane Ibrahaim Kaduma &**

**Another,** Commercial Case No. 128 of 2019, HC- Dar es Salaam ambapo amri ilitolewa stamp duty ilipwe kwenye uamuzi wa pingamizi na sio kwenye hukumu ya kesi ya msingi. Hivyo hukumu hiyo imenukuliwa vibaya. Alidai ilipaswa kuamuriwa mikataba yote ambayo haijalipiwa isipokelewe kama kifungu 47 cha sheria tajwa kinavyoainisha. Alisisitiza amri iliyotolewa na Mahakama ya wilaya kuelekeza mikataba iliyokwisha pokelewa ilipiwe ushuru wa forodha.

Bw. Machibya alipojadili sababu ya 2 alieleza Mahakama ya Rufaa ya kwanza ilikosea kisheria na kimantiki kwa kutambua nyaraka za mauziano, hali zikiwa zimebadilishwa tarehe na alisema kama alivyo wasilisha katika hoja ya 3 kwamba mikataba hiyo haikuwa na ushuru wa forodha "stamp duty" na isingepaswa kupokelewa kama kielelezo cha kesi.

Katika sababu ya 4 wakili Machibya alisema kwamba maelezo yaliyotolewa na mashahidi yalibadilishwa katika hukumu ambapo alidai kwamba katika mahakama ya mwanzo shahidi alisema kwamba wadaawa walipata mtoto aitwae Ashura Lukoro Juma, akirejea ushahidi wa (SU2) Zainabu Mussa Hamis. Pia maelezo ya fremu nne za maduka yaliyoko Sagara, nyumba (apartments) 3 zilizoko Sagara, duka la JB Spare Parts, Don Car Parking-Tabata, na Nyumba tano zilizoko Buroge Kigoma hazikuorodheshwa.

Katika sababu ya 7 alieleza Mahakama ya Wilaya ilikosea kisheria na kimantiki kwa kutotoa amri ya kufanya DNA kulingana na mamlaka yake chini ya kifungu 108(c) Sheria ya Ndoa, ili kutoa amri ya matunzo na nani ataishi na mtoto huyo. Wakili Machibya alieleza kwamba katika shauri Na. 271 la 2022 Mahakama iliyosikiliza shauri haikutoa amri ya kufanyika vipimo vya DNA ili kujua nani akae na mtoto ukizingatia mtoto husika alizaliwa tarehe 19/08/2018 na ndoa ilifungwa tarehe 16/09/2017.

Akiendelea kujadili sababu ya 9 wakili Machibya alidai mahakama ilikosea kutotoa amri ya shauri kusikilizwa upya ili kuwapa nafasi mashahidi walioitwa na mahakama ili kuthibitisha upatikanaji wa mali na maboresho yake. Alieleza zaidi kuwa katika ukurasa wa 18 na 19 wa hukumu ya mahakama ya mwanzo mashahidi ambao ni mafundi na wenyeviti wa vijiji waliitwa na mahakama lakini hawakupewa nafasi ya kusikilizwa.

Katika sababu ya 10 wakili Machibya alidai kwamba, mrufaniwa aliamuriwa kulipa matunzo ya Tsh. 150,000/= kwa mwezi sawa na jumla ya Tsh 3,150,000/= ambayo ni fidia ya matunzo kwa miezi 21 kuanzia Machi, 2021 talaka tatu zilipotolewa. Pia mrufani alidai kwamba Tsh. 150,000/= ni ndogo kwa kuzingatia kipato cha mrufaniwa ambaye anafanya kazi GF Trucks and Equipment's kama Afisa Masoko na mshahara wake kwa mwezi ni Tsh. 2,328,720/- kabla ya makato. Aliiomba mahakama iamuru amri ya matunzo kiasi cha Tsh. 500,000/= kwa mwezi.

Wakili Machibya alimalizia mawasilisho yake ya sababu ya 1 ambapo alidai mahakama ya kwanza ya rufaa ilikosea kimantiki na kisheria kwa kutozingatia kuwepo kwa utofauti wa namba ya shauri kwenye hukumu na wito wa tarehe 03/03/2022 kutofanana kinyume cha kisheria. Hivyo aliiomba mahakama hii ikubali rufaa yake.

Katka majibu ya hoja na mawasilisho yaliwasilishwa na wakili Paulo Patience Hyera kwa niaba ya mrufaniwa alianza kwa kusema, kutokana na amri ya tarehe 12/09/2023 mrufani alitakiwa kuwasilisha hoja zake kabla ya tarehe 19/09/2023 lakini yeye alileta tarehe 20/09/2023 hivyo hoja zipo nje ya muda.

Alieleza zaidi kuwa katika hoja za mrufani anapinga maamuzi ya Mahakama ya Wilaya lakini katika mawasilisho yake anapinga hadi yale ya Mahakama ya Mwanzo jambo ambalo halipo sawa kisheria.

Akianza kujibu hoja zilizowasilishwa, wakili Hyeraa alisema kwamba mahakama haikukosea kupunguza fidia ya Tsh. 8,670,000 kwa sababu hakukuwa na mkataba wa kuthibitisha uhalali wa kodi hiyo.

Ilikua ni rai ya wakili Hyera kwamba wadaawa walipokuwa wakiishi pamoja mrufaniwa alikua akilipa pango la Tsh. 150,000/=. Hivyo amri ya kulipwa Tsh 5,250,000/= ikiwa ni kodi ya miezi 21 kwa pango la Tsh 250,000/= kwa mwezi haikuwa sahihi.

Akijibu hoja za sababu ya 5, 6, na 8 ambapo mrufani alidai mgao sawa wa mali za ndoa na alizomkuta nazo mrufaniwa. Wakili Hyera alisema mahakama inapaswa tu kuangalia mchango wa kila mwanandoa aliouchangia katika upatikanaji wa mali hizo katika kufanya mgao wa mali za ndoa. Aliielekeza mahakama katika shauri la **Yesse Mrisho dhidi ya Sonia Abduli,** Mahakama ya Rufaa, ukurasa wa 9 na 10. Ambapo katika shauri tajwa mrufaniwa alitakiwa kuthibitisha mchango wake katika mali za ndoa.

Pia alipinga hoja ya kugawa mali sawa katika ndoa yenye wake wengi bila kuangalia mchango wa mwanandoa kuwa ni dhaifu na yenye kupotosha. Wakili Hyera alieleza ndoa baina ya wadaawa ilifungwa tarehe 16/09/2017 na waliachana Kiislamu tarehe 17/05/2019 hivyo kudumu kwa miezi 15 tu. Mrufani akiwa ni mke wa pili na hakukuwa na machumo yeyote ya pamoja. Aliongeza kwa kusema amri ya kugawana gari aina ya Toyota Vitz ilikua ni batili kwakuwa ilinunuliwa tarehe 28/2/2020 kipindi ambacho hawaishi pamoja.

Katika hoja ya 3 kuhusu kupokelewa mkataba bila kuwa na ushuru wa forodha "stamp duty", wakili Hyera alijibu kwamba ni kweli mbele ya Mahakama ya Mwanzo mikataba ya mauziano ilipokelewa bila kuwa na stamp duty na Mahakama ya Wilaya ilitoa amri kwamba mjibu rufaa alipie stamp duty ili ipate nguvu kisheria kwakuwa sheria inaruhusu. Akirejea

uamuzi katika shauri la **Mohamed Abood as Attorney of Walid Abood Salehe dhidi ya D.F.S Salehe Express Lines Limited,** Mahakama ya Rufaa Tanzania, Dar es Salaam, ukurasa wa 12 na 13.

Akijibu sababu ya 4, kwamba mahakama ilikosea kisheria kwakuwa maelezo ya mashahidi yalibadilishwa kwenye hukumu. Wakili Hyera alisema mahakama ya wilaya sio iliyosikiliza ushahidi hivyo kuwa ni hoja iliyopotoka.

Katika hoja ya 7 ilikua ni rai ya wakili Hyera kuwa mbele ya mahakama kulikuwa na shauri la talaka na sio maombi ya DNA ambayo mrufani anaweza kuyawasilisha katika Mahakama ya Watoto na kuomba vipimo vya vinasaba.

Hoja ya 9 Bw. Hyera alifafanua kwamba hoja ya kwamba mashahidi hawakupewa muda wa kusikilizwa nayo haina mashiko kwani kiini cha kesi ni talaka ambayo haikupingwa na katika Mahakama ya Mwanzo mrufani alikuwa na muda wa kuleta mashahidi.

Katika hoja ya 11, iliyohusu uamuzi wa mahakama ya kwanza ya rufaa kutoa amri ya matunzo katika kipindi cha miezi 21 kwa mwezi ikiwa ni Tsh. 150,000/- na kuleta jumla ya Tsh. 3,500,000/- Bw. Hyera alieleza kuwa amri hiyo haikuwa na kosa lolote.

Wakili Hyera katika hoja za sababu ya 1 iliyodai kuna namba tofauti ya shauri iliyoandikwa katika wito na shauri husika, alieleza kwamba hakukuwa na kosa kwani mrufani aliweza kujua uwepo wa shauri na kosa hilo likiwa ni la kiuandishi nafuu yake ni mapitio na sio rufaa.

Wakili Hyera alihitimisha kwa kueleza rufaa hii haina mashiko na hivyo mahakama hii itupilie mbali kwa gharama.

Mahakama baada kupitia hoja ndefu za wadaawa kuhusiana na rufaa hii, kabla ya kujadili sababu hizo za rufaa ni vema kueleza mapema kuwa

hii ni mahakama iliyoketi kwa rufaa ya pili. Hivyo haina wajibu wa kuingilia maamuzi ya mahakama mbili za awali, hasa kwenye hoja ambazo tayari kuna maamuzi yanayoshabihiana baina ya mahakama iliyoamua shauri hiyo na iliyoketi kwenye rufaa ya kwanza. Isipokua tuu kama kuna ukiukwaji wa sheria au kutojielekeza vema katika ushahidi uliotolewa kama ilivyoelezwa kwenye kesi ya **Helmina Nyoni dhidi ya Yeremia Magoti** (Civil Appeal No. 61 of 2020) [2022] TZCA 170.

Pia kabla ya Kwenda kwenye kiini cha rufaa hii, kupitia mawasilisho ya majibu ya sababu za rufaa wakili Hyera ameeleza kwamba mawasilisho ya hoja haya yamechelewa ikiwa ni kinyume na amri ya tarehe 12/09/2023 ambayo ilimtaka mrufani alete hoja za kufafanua sababu za rufaa yake kufika tarehe 19/9/2023, lakini aliziwasilisha tarehe 20/9/2023. Hoja hii haitajadiliwa kwani jambo hili mahakama ilishalitolea uamuzi tarehe 19/4/2024 katika maombi madogo Na. 1086 ya 2024, ambapo mahakama hii ilitengua amri ya kutupilia mbali shauri Na. 23 ya 2023 iliyotoa hapo awali na kuruhusu kurejesha shauri hili kusikilizwa.

Nikirejea katika sababu za rufaa zilizowasilishwa, baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili na kupitia kumbukumbu za shauri husika, nitajadili sababu hizo kwa kuanza na sababu ya 10 na 11 kwakuwa zinashabihiana, ikifuatiwa na ya 5, 6 na 8 kwa pamoja ambazo pia zinashabihiana, na sababu zingine ikiwa ni 1, 2, 3, 4, 7, 9 kwa upekee.

Nikianza kujadili sababu ya 10 na 11 za rufaa hoja kuu inayo bishaniwa hapa ni fidia ya pango kwa kipindi cha miezi 36 kwa Tsh. 8,670,000/- mpaka tarehe ya hukumu ya talaka ilipotolewa. Pamoja na matunzo kwa miezi 36 kiasi cha Tsh. 5,400,000/= mpaka tarehe ya hukumu ya talaka ilipotolewa.

Katika sababu hizi za rufaa majumuisho makuu mrufani hana pingamizi dhidi ya hakimu wa Mahakama ya Wilaya pale alipo amuru

mauzo ya gari aina ya Toyota Vitz yasitumike katika kulipia fidia hizo, kwani itapoka hake ya mrufaniwa ya mgao wa mali ya ndoa.

Wakili Machibya amesisitiza kuwa mahakama ya wilaya ilipaswa kutoa fidia kutoka kipindi mrufani ametelekezwa mpaka tarehe ya hukumu ya talaka ilipotolewa ikiwa ni miezi 36 badala ya 21 iliyotoa mahakama ya wilaya. Alidai kiwango cha matunzo ya Tsh. 150,000/- kilikua kidogo kulinganisha na kipato cha mrufaniwa. Kwa upande wa wakili Hyera anaafiki kiwango cha matunzo kama ilivyoamriwa na mahakama ya wilaya lakini anapinga kiwango cha pango kuwa sio halisi.

Katika kuangalia mawasilisho ya pande zote mbili, upande wa mrufaniwa haupingi kulipa fidia hizo, isipokuwa kinachopingwa ni kiwango cha pango tu. Msingi wa mahakama ya wilaya kutoa fidia ya kwa miezi 21 ilieleza ni kutoka kipindi talaka ya Kiislamu ilipotolewa na mrufaniwa kuanzia June, 2019 mpaka Machi 2021. Katika hukumu ya mahakama ya wilaya ilieleza kuwa talaka ilitolewa Machi, 2021 tofauti na talaka ya kiislamu iliyowasilishwa mahakamani kama kielezo.

Aidha, msingi wa mrufani kudai fidia hizo ni kwamba alitelekezwa na mrufaniwa, akiwa amepewa talaka tatu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Mpaka talaka hiyo ilipothibitishwa na mahakama kwa hukumu ya tarehe 30/6/2022.

Kwa kuzingatia fungu 115(1) (f) la Sheria ya Ndoa, linairuhusu mahakama kutoa amri ya matunzo pale wadaawa wanapokua walifunga ndoa ya Kiislamu. Mke hustahili kupewa matunzo katika kipindi cha eda tu (Iddat) kama fungu hilo linavyoeleza;

*115. (1) The court may order a man to pay maintenance to his wife or former wife–*

*(f) where the parties were married in Islamic form, for the customary period of iddat following the date on which the divorce takes, or is deemed to have taken, effect;*

Kwa kuzingatia matakwa ya dini ya Kiislamu ambayo wadaawa walifunga ndoa na kuishi kwa kufuata imani hiyo, matunzo yalipaswa kutolewa kwa kipindi cha miezi mitatu baada ya talaka ya Kiislamu kutolewa ili mke akae katika kipindi cha eda. Mahakama hii haioni uhalali wa fidia ya kipindi cha miezi 21 iliyotolewa na mahakama ya wilaya kufidia pango la nyumba. Hivyo mahakama hii inabadili uamuzi wa mahakama ya wilaya na kutoa fidia ya pango ya Tsh. 750,000/- kwa kipindi cha miezi 3 kwa kodi ya Tsh. 250,000/- kwa mwezi.

Katika upande wa matunzo ya mtoto, kwa kupitia hukumu ya mahakama ya wilaya na hoja zilizowasilishwa, hakuna ubishi kuwa talaka tatu za Kiislamu zilitolewa tarehe 17/5/2019 na talaka ya kimahakama itolewa tarehe 30/6/2022. Hivyo ni dhahiri kuwa matunzo kwa mtoto yaliyopaswa kutolewa ni kwa kipindi cha miezi 36 na sio 21 kama mahakama ya wilaya ilivyoamua.

Nikirejea katika hoja ya kiwango cha matunzo ambapo upande wa mrufani amedai Tsh. 150,000/- ni kiasi kidogo kulingana na kipato cha mrufaniwa. Mahakama hii inazingatia kuwa pande zote katika hoja zao wameeleza mrufani alikua na familia nyingine ya mke wa kwanza. Ni rai ya mahakama kuwa kwa kiwango kilichotolewa kwa Tsh. 150,000/- kwa mwezi na kupitishwa na mahakama zote mbili za chini, haioni sababu ya kubadili kiwango hicho, isipokuwa haikubaliani na fidia ya miezi 21 bali kwa miezi 36. Hivyo sababu ya rufaa Na. 10 na 11 zina mashiko kwa sehemu na zimebadirishwa kiwango cha fidia kwa kiasi ambacho kimeelezwa katika hoja hizi.

Katika sababu ya 5, 6 na 8 ambayo inahusu mgawanyo wa mali zilizotokana na machumo ya ndoa na maboresho au kuendelezwa na upande mwingine. Katika Sheria ya Ndoa, ipo wazi katika kifungu cha 114(2) (b) kwamba Mahakama katika kugawanya mali itazingatia mchango wa kila mwanandoa.

Mrufani amekiri kukuta baadhi ya mali katika majumuisho yake lakini amedai kwamba sheria inataka kugawana kwa usawa baina ya wake wote bila kuangalia lini mtu aliolewa au uwepo wa mke mwingine. Kwa upande mwingine mrufaniwa akidai katika miaka 2 ya ndoa yao hawakuchuma mali yoyote.

Katika shauri hili, hakuna ubishi kuwa mrufaniwa alikuwa na mke zaidi ya mrufani kwa mujibu wa ndoa yao ya Kiislamu. Ambapo kimisingi ndoa ya kiislamu inatambua uwepo wa zaidi ya mke mmoja. Aidha, katika kugawa mali kwa waliokuwa wanandoa, kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa, Mahakama itaangalia mchango wa kila mke katika upatikanaji wa mali. Katika shauri la **Gabriel Nimrod Kurwijila vs Theresia Hassan Malongo** (Rufaa Madai Na. 102 of 2018) [2020] TZCA 31 Mahakama ya Rufani ilieleza kuwa mahakama itaangalia ushahidi uliowasilishwa na pande zote mbili katika kuthibitisha mchango wa machumo wa mali za pamoja za ndoa.

Katika kumbukumbu za shauri kama alivyosema hakimu wa wilaya, wadaawa walianza kwa kuishi katika nyumba ya kupanga na hakuna mali iliyothibitika kwa kuchuma pamoja isipokuwa gari Toyota vits. Mahakama ya wilaya iliona hakuna uthibitisho wa maboresho au mchango wa mali nyingine ya ndoa, bali kulikuwepo uthibitisho wa mali binafsi za mrufaniwa za mrufaniwa.

Kugawa mali zingine ambazo mrufani alizikuta kwa mrufaniwa akiwa na mke mwingine ni dhuluma ya jasho ambalo mrufani hana mchango wa

mali hizo. Hili pia liliwahi kusemwa katika shauri la **Mwamoi Shehe Mtikuu vs. Isa Matala Mduma**, Rufaa Madai Na. 72 ya 2020, Mahakama Kuu iliyoketi Temeke.

Kwakuwa kuna uthibitisho wa gari aina ya Toyota Vits kuwa mali ya Pamoja ya ndoa ninaafiki mgao ambao iliamriwa na mahakama ya wilaya kwa mrufani kupata mgao wa asilimia 40% na mrufaniwa 60% baada ya kufanyiwa tathimini ya thamani na kutoa gharama za mauzo na kodi stahiki.

Katika mali nyingine mahakama hii inaona kwamba hakuna ushahidi mwingine uliothibitishwa ambao unaweza kutengua maamuzi ya wilaya hivyo sababu hizi kukosa mashiko.

Nikienda katika sababu ya 3 ya rufaa ambapo mrufani anapinga kupokelewa kwa mikataba ya mauziano kama kielelezo pasipo kuwepo ushuru wa forodha (stamp duty). Pasipo kupoteza muda, ninaafiki hoja za hakimu wa wilaya kuamuru pande hizo kutimiza takwa la kisheria kwani haliathiri utoaji wa haki bali ni utaratibu ambao madhara yake hayaendi kuaathiri kiini cha kesi. Katika kesi ya **Mohamed Abood as Attorney of Walid Abood Salehe vs D.F.S Salehe Express Lines Limited**, (iliyotajwa hapo juu) mahakama iliona ili kutenda haki, inaweza kuruhusu mkataba kulipiwa ushuru wa forodha baada ya kupokelewa kama kielelezo. Sababu hii inakosa mashiko na kutupiliwa mbali.

Sababu inayofuatia kujadiliwa ni ile ya 9 ambayo mrufani anadai ilipaswa shauri kurudi kusikilizwa upya kwa kuwapa nafasi mashahidi walioitwa kutoa ushahidi wao. Mahakama ya wilaya imeeleza kuwa mrufani alipewa muda wa kutosha kuleta mashahidi lakini alishindwa kuwaleta kwa wakati. Sababu hii ni dhaifu, mrufani alipewa haki ya kuleta mashahidi na alishindwa kufanya hivyo, na hiyo sio sababu ya kufanya shauri hili liamriwe kusikilizwa upya, sababu hii pia haina mashiko na inatupiliwa mbali.

Sababu ingine ya 7 ni inayohusu suala la vipimo vya vinasaba (DNA). Katika sababu hii, nina afiki uamuzi wa mahakama ya wilaya ambapo mbali na kukubaliana na amri ya matunzo iliyotolewa na mahakama ya mwanzo kwa mtoto. Hoja ya kutaka vifanyike vipimo vya kinasaba kuthibitisha mtoto ni wa mrufaniwa, wadaawa bado wanayo nafasi kupeleka maombi hayo katika mahakama husika kwa ajili ya kujua mustakabali wa jambo hilo.

Kwa mahakama za chini kutokutoa amri hiyo, haijaleta athari katika shauri hili. Hivyo sababu hiyo pia haina mantiki na inatupiliwa mbali.

Nikigeukia katika sababu ya rufaa ya 4 inayodai ushahidi uliotolewa mbele ya mahakama kulibadirishwa katika hukumu. Mahakama hii imebaini makosa ya uandishi wa namba ambayo yangeweza kurekebishwa kwa marejeo lakini hayakuleta athari kwa kutokutenda haki katika pande zote husika.

Hoja za Ushahidi mwingine kutoandikwa unakosa mashiko kwakuwa mahakama ilichambua ushahidi wa pande zote mbili katika hukumu ya shauri hilo. Kadhalika hoja hii inakufa kwa kukosa mantiki na inatupiliwa mbali.

Katika sababu ya 1 ya rufaa ambapo mrufani anakosoa kunukuliwa vibaya kwa namba ya kesi ya msingi kutoka mahakama ya mwanzo katika rufaa ya mahakama ya wilaya. Katika hoja zilizowasilishwa nakubaliana na hoja ya wakili Hyera kuwa kosa la kiuandishi lilipaswa kurekebishwa kwa njia ya marejeo na sio rufaa kwakuwa haiathiri msingi wa shauri husika na haki za wadaawa. Sababu hiyo haina budi pia kutupiliwa mbali.

Kwa kuhitimisha na sababu ya rufaa ya 2 inayodai nyaraka za mauziano zilizotolewa mahakama zilibadirishwa tarehe za manunuzi na mahakama ilishindwa kutoa uamuzi katika hoja hiyo. Hoja hii kwakuwa haikujadiliwa na mahakama ya wilaya na iliwasilishwa kama sehemu ya

sababu za rufaa, mahakama hii ikiingia katika viatu vya mahakama hiyo inaona kwamba katika vielelezo vilivyowasilishwa hakukuwa na kiashiria cha vielelezo hivyo kugushiwa kama mrufani anavyodai na kwakuwa hakutoa ushahidi mwingine kuthibitisha uwepo wa nyaraka halisi za awali mahakama haiwezi kuchukua ushahidi mwepesi kuthibitisha kuwepo kwa kugushi hoja yenye viini vya jinai. Hivyo pia sababu hii inakufa kwa kukosa mashiko na inatupiliwa mbali.

Baada ya kupitia sababu zote za rufaa, mahakama inaona kuwa rufaa hii imefanikiwa kwa sehemu tuu katika kiwango cha fidia ya matunzo kuwa Tsh. 150,000/- kwa miezi 36 badala ya 21 kwa jumla ya Tsh. 4,650,000/- lakini pia kutoa fidia ya malazi kwa miezi mitatu tu ya kipindi cha Iddat kwa kiwango jumla ya Tsh. 750,000/-. Uamuzi mwingine utabaki kama ilivyoamriwa na mahakama ya wilaya.

**Imetolewa** hapa **Dar es Salaam** leo tarehe 22 Mei, 2024

**G.N. BARTHY**

**JAJI**

Hukumu hii imetolewa leo mbele ya Bw. Emmanuel Machibya wakili wa upande wa Mrufani, Bw. Paulo Hyera wakili wa upande wa Mrufaniwa na Mrufaniwa binafsi